

## **KAZI YA ZIADA- KIDATO CHA KWANZA**

### **SEHEMU A ( SARUFI- ISIMU) -WIKI 1-WIKI 4 ( 21 NOV-30 NOV 2024)**

1. Eleza maana ya vipashio vifuatavyo huku ukitolea mifano ( al 6);

☒ Viambishi

☒ Silabi

☒ Mzizi wa kitenzi

2. Andika vitenzi vifuatavyo katika kauli ya kutendewa ( al 8)

☒ Kamata

☒ Choma

☒ Koma

☒ Gongga

3. Changanua sentensi ifuatavyo kwa njia ya matawi ( al 9)

☒ Mama ameniandalia mchuzi wa pweza mtamu

☒ Mpira wangu umeshonwa jana asubuhi

☒ Wewe umekaribshwa katika sherehe yangu

4. Onyesha udogo na ukubwa wa nomino zifuatazo katika sentensi ( al 6)

☒ Mtoto amebeba kitabu kwenye mkoba

☒ Kikombe cha mwanafunzi kiko kwenye meza

☒ Mtu ameepua chungu kutoka mekoni

5. Kwa kutumia mchoro wa ulimi onyesha utamkaji wa irabu za Kiswahili  
( al 6)

6. Tambua mahali ambapo konsonanti zifuatazo hutamkiwa

/ny/, /ng/, /h/, /sh/, /n/

7. Ainisha vigezo vitatu vya kuanisha konsonanti za Kiswahili ( al 3)

8. Tunga sentenzi mbili zenye miundo ifuatayo ya maneno ( al 6)

☒ N+V+T+E+N

☒ E+V+T+E+E

☒ H+T+N+V

9. Tunga sentensi ukitumia vivumishi vimilikishi vitatu ( al 6)

@Edwin Johnson Akal FM 1W@ St Mary`s Girls @ Mr Peter Mutune Fm IP

10. Eleza tofauti kati ya sauti ghuna na sauti sikhuna huku ukitolea mifano

kwa kila ( al 4)

11. Chora jedwali linaloonyesha konsonanti za Kiswahili zote na ala

mbalimbali zinapotamkiwa ( al 14)

12. Eleza tatu bainifu za irabu zifuatazo /e/, /u/, /o/ na /a/

13. Ainisha aina tano za nomino na utolee mifano kwa kila ( al 10)

14. Ainisha miundo minne ya irabu za Kiswahili ( al 8)

15. Eleza maana ya silabi mwambatano ( al 2)

16. Andika mifano mitatu ya silabi mwambatano

WIKI 1 Desemba- WIKI 4 Desemba 9 ISIMU JAMII NA FASIHI

17. Eleza kaida sita zinazothibiti matumizi ya lugha katika jamii ( al 12)

18. Ainisha dhima sita za lugha katika jamii ( al 12)

19. Fafanua sifa tano za lugha ( al 10)

20. Ainisha sifa tano za sajili zifuatazo

☒ Sajili ya hospitalini

☒ Sajili ya kituo cha basi

☒ Sajili ya kituo cha polisi

Fasihi simulizi

21. Eleza tofauti sita kati ya Fasihi Andishi na Fasihi simulizi ( al 12)